TAASISI YA USTAWI WA JAMII

HUDUMA HUKUZA MAENDELEO

**CHUO CHA USTAWI WA JAMII**

DAR ES SALAAM & KILIMANJARO




# JARIDA LA MTANDAONI

**OKTOBA - DESEMBA, 2024**



Mkuu wa Chuo Dr. Joyce Nyoni akitoa hotuba katika kilele cha Wiki ya Usajili na Mafunzo ya Awali kwa Wanafunzi wapya kwa mwaka wa masomo 2024/2025

# USAJILI WA WANAFUNZI WAPYA MWAKA WA MASOMO 2024-2025

**Mkuu wa Chuo Dkt Joyce Nyoni, tarehe 25 Oktoba 2024 alitamatisha majuma mawili ya wiki ya Usajili na mafunzo ya awali kwa wanafunzi wapya kwa mwaka wa masomo 2024/2025 ambapo aliwaasa wanafunzi kusoma kwa bidii na kutimiza malengo yaliyowaleta chuoni, akisisitiza mabinti kutoanzisha mahusiano ambayo yatawatoa kwenye malengo makuu ya kufikia ndoto zao na kuongeza kuwa Kila mwanafunzi kuhakikisha analinda taswira nzuri ya chuo kwa kuwa wanafunzi wenye tabia njema ndani na nje ya chuo.**



Wanafunzi wapya kwa mwaka wa masomo 2024/2025 wakiwa wanasajiliwa kujiunga na Chuo cha Ustawi wa Jamii



Mkuu wa Chuo Dkt Nyoni akikagua ujenzi wa madarasa mapya unaoendelea katika kampasi ya Dar es Salaam akiwa pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo Utawala Dkt Mugyabuso (katikati) na Msanifu majengo - Mark (Kushoto)

## UKAGUZI WA UJENZI WA MADARASA

**Mkuu wa Chuo, Dkt. Joyce Nyoni alifanya ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa madarasa mapya unaoendelea katika kampasi ya Dar es Salaam tarehe 1 Oktoba 2024, ambapo ujenzi unatarajiwa kukamilika rasmi mwanzoni mwa mwaka 2025. Mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya kujifunzia katika kampasi ya Dar es Salaam**



Picha ya muonekano wa juu, ujenzi wa madarasa mapya ukiendelea




Mkuu wa Chuo Dkt Nyoni (Kushoto) akipokea Tuzo ya NBAA

## TUZO NBAA (ISW YAIBUKA MSHINDI WA PILI UANDAAJI WA HESABU ZA FEDHA TUZO ZA NBAA)

**Chuo cha Ustawi wa Jamii kimeibuka mshindi wa pili kwenye uandaaji wa hesabu za kifedha zinazozingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu katika kundi la vyuo vya elimu ya juu. Tuzo hizo zilitolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) Novemba 29, 2024, Jijini Dar es Salaam.**




Tuzo ya mshindi wa pili kwenye uandaaji wa hesabu za kifedha zinazozingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu kundi la vyuo vya elimu ya juu.




Mshauri wa Wanafunzi Chuo cha Ustawi wa Jamii Dkt. Andrew Randa akizungumza na wanafunzi katika maadhimisho siku ya watu wenye Ulemavu Duniani

## MAADHIMISHO SIKU YA WATU WENYE ULEMAVU DUNIANI

**Chuo cha Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na serikali ya wanafunzi (ISWOSO), tarehe 3 Desemba 2024, kiliadhimisha siku ya watu wenye ulemavu duniani kwa kuzindua umoja wa wanafunzi wenye ulemavu wa vyuo vikuu (USU-PSN). Umoja huo ulizinduliwa na Mgeni rasmi, Dkt Andrew Randa, Mshauri wa Wanafunzi**



Wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii katika Maadhimisho siku ya watu wenye ulemavu duniani

**Uzinduzi huo pia uliambatana na utoaji wa tuzo kwa watu waliotoa mchango mkubwa kwa ustawi wa watu wenye mahitaji maalum, hatua iliyolenga kutambua na kuhamasisha juhudi za kuimarisha ushirikishwaji wa watu wenye mahitaji maalum**



Wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii katika Kongamano la 11 la Kitaaluma

## KONGAMANO LA KITAALUMA (CONVOCATION)

**Chuo cha Ustawi wa Jamii kimekuwa na utamaduni wa kufanya kongamano la kitaaluma (Convocation) kila mwaka kabla ya mahafali. Tarehe 5/12/2024 Chuo cha Ustawi wa Jamii kilifanya kongamano la 11 la kitaaluma(convocation) juu ya uwezeshaji na ubunifu katika kubadilisha elimu kuwa fursa. Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma Prof. Sotco Komba alieleza kuwa Kongamano hilo la kitaaluma limekuwa ni fursa kwa wanafunzi kujifunza na kuelewa dhana nzima ya ubunifu.**



Wahitimu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Katika Mahafali ya 48 & 7 ya Chuo cha Ustawi wa Jamii

## MAHAFALI YA 48 & 7

**Chuo cha Ustawi wa Jamii kilifanya mahafali yake ya 48 kwa kampasi ya kijitonyama na mahafali ya 7 kwa kampasi ya Kisangara yaliyofanyika katika viwanja vya Chuo cha Ustawi wa Jamii Dar es Salaam tarehe 11/12/2024. Mgeni rasmi katika mahafali hayo akiwa ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dkt. Dorothy Gwajima (Mb). Kwa Mwaka wa Masomo 2023/2024 Chuo kimetoa wahitimu 3112 ambao asilimia 65.5 ni wanaume na asilimia 34.6 ni wanawake.**



@isw_official_tz @isw_official_tz @taasisiyaustawi @isw_official_73 www.isw.ac.tz


Mkuu wa Chuo Dkt Joyce Nyoni akizindua muongozo wa ufanyaji Tafiti utakaotumiwa na Kamati ya Maadili ya Tafiti ISWREC

# UZINDUZI WA KAMATI YA MAADILI YA KITAFITI- ISWREC

**Chuo cha Ustawi wa Jamii kimezindua kamati ya Maadili ya Tafiti (Institute of Social Work Research Ethics Committee-ISWREC) katika hafla maalum iliyofanyika katika kampasi ya Kijitonyama, Dar es Salaam Desemba 12, 2024. Sambamba na uzinduzi wa kamati hiyo Mkuu wa Chuo Dkt Joyce Nyoni , kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Tafiti (ISWREC) Dr Joyce Ikingura walizindua muongozo wa ufanyaji wa tafiti ambao utatumika kama muongozo wa kuhakikisha tafiti zote zinazofanyika katika Chuo cha Ustawi zinazingatia maadili ya kitafiti.**

**Uzinduzi wa ISWREC unadhihirisha dhamira ya Chuo cha Ustawi wa Jamii katika kuhakikisha tafiti za kitaaluma zinafanyika kwa njia inayoheshimu maadili ya kitafiti na haki za washiriki katika kuchangia maendeleo ya kijamii na kitaaluma**


Picha ya pamoja kati ya Uongozi wa Chuo cha Ustawi wa jamii na Kamati ya Maadili ya Tafiti ISWREC




Mhadhiri Msaidizi Juliana Mheluka akitoa huduma kwa wananchi waliotembelea banda la Chuo cha Ustawi wa Jamii katika Tamasha la Kimataifa la Maendeleo ya Filamu na Sanaa

# TAMASHA LA KIMATAIFA LA MAENDELEO YA FILAMU NA SANAA

**Chuo cha Ustawi wa Jamii Kilishiriki Tamasha la kimataifa la Maendeleo ya Filamu na Sanaa ambapo wanafunzi wa chuo Ustawi wa Jamii wamepata nafasi ya kushiriki katika mdahalo kuhusu Jinsia na Sanaa, mdahalo ulioitwa "Binti Longa Gender" na Kubadilishana mawazo na wasanii na wawezeshaji katika mdahalo huo.**

**Tamasha hilo ambalo lilianza tarehe 11 Desemba na kuisha tarehe 15 Desemba 2024 lilifanyika katika viwanja vya Posta Kijitonyama Dar es Salaam.**



Wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii waliohudhuria katika mdahalo wa “ Binti Longa Gender “ katika Tamasha la Kimataifa la Maendeleo ya Filamu na Sanaa




Watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Kampasi ya Kisangara katika Mwanga Festival and Marathon 2024

# MWANGA MARATHON

**Watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kampasi ya Kisangara, wameshiriki katika Mwanga Festival and Marathon 2024, tukio lililofanyika tarehe 27 Desemba 2024 katika Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro. Mbio hizo zilifunguliwa rasmi na RAS wa Kilimanjaro Kiseo Yusuf Nzowa pamoja akiambatana na Mkuu wa Wilaya ya Mwanga Mhe. Mwanahamisi Munkunda.**

**Kwa kauli mbiu ya 'Run for Fun on Season Festivals,' tukio hili lililenga kuhamasisha mazoezi, afya bora, mshikamano wa kijamii, na kuendeleza utalii wa ndani katika Wilaya ya Mwanga.**

# CHUO CHA USTAWI WA JAMII

Institute of Social Work
210 Shekilango Road
P.O. BOX 3375
14113 Kijitonyama
Dar es Salaam
+255735509090
+255677111200
+255716121096
rector@isw.ac.tz
or
info@isw.ac.tz